WASIFU WA SHEIKH AL-MUHADDITH ;
ALI HASAN IBN ABDULHAMID AL-HALABI

Nasaba Yake:

Ni mwanachuoni wa ki-salafi, anayeshikamana na kufuata athar (riwaya), mwandishi na muhaqqiqi wa vitabu chungu nzima vya kiislaamu: Ali ibn Hasan ibn AbdulHamid Al-Yaafi (mji anapotaka asili ; mji wa Jaffa huko Falastin), Al-Halabi (mji wa nasaba huko Aleppo, Syria), Al-Urduni (mji walioshukia na kukaa wazee wake baada ya kufanya Hijra kutoka Falastin).

Anajulikana kama Abul-Harith.

Kuzaliwa Kwake:

Alizaliwa mjini Zarqaa, Jordan ; siku ya 29 Jumaadaa at-Thaani, 1380 Hijri.

Mzee wake na babu yake walihama kutoka Jaffa, Palastina -mwaka 1948- kwa sababu ya vita na ufisadi wa mayahudi – laana ya Allaah iwafikie.

Kukulia Kwake Na Kutafuta Ilm, Na Walimu Wake:

Alianza kutafuta ilimu takriban alipopita miaka ishirini wa umri wake.

Katika waalimu wake maarufu kabisa ni :

1. Mwanachuoni mkubwa, Muhaddith, Shaykh Muhammad Naasir-ud-deen Al-Albaani (rahimahullaah)

Alikutana na Sheikh Al-Albaani katika mwisho wa mwaka 1977 huko Jordan, na akaanza kuambatana naye akinywa kutoka hiyo bahari ya ilimu na adabu za Sunnah. Hivyo akawa mwanafunzi wa sheikh Al-Albaani hadi kifo chake.

2. Mwanachuoni wa lugha ya kiarabu, Shaykh AbdulWadood az-Zaraari (rahimahullaah).

3. Alikutana na wanavyuoni wengi –miji tofauti- ambao walimtunuku na ijaazah za tazkiya (Uthibitisho wa ki-ilimu) ili awe na uwezo wa kufundisha na kupokea hadeeth kutoka kwao. Miongoni mwa baadhi ya wanavyuoni hao ni Sheikh Badee' ar-Raashidee (muhaddith wa Sind),

Sheikh Muhammad as-Saalik as-Shanqiti, na Sheikh Hammaad al-Ansaaree (Muhaddeeth wa Madeenah).[1]

Sifa alizopewa na Ma Ulamaa [Wanachuoni wakubwa] wa Sunna:

1. Al-Imaam sheikh Abdulazeez ibn Baaz (rahimahullaah)

Sheikh Ibn Baaz (rahimahullaah) alimtunuku sheikh Ali kwa kumuandikia utangulizi wa kitabu chake thabiti: *'Innahaa Salafiyya Aqidatun wa Manhaj.'*

2.Imaam Muhammad ibn Swaaleh al-Uthaymeen (rahimahullaah)

Alisema shaykh Abu Twalha Umar ibn Ibraahim: 'Alinihadithia Ahmad ibn Ismail, aliysema: 'Alinihadithia Abu Abdullaah Qamaru-z-Zaman al-Pakistaani as-Salafi (mwalimu katika madaaris al-manaarat Jeddah) alisema:

'Katika msimu wa hajj ya mwaka 1420 Hijri, Alikuwa Imaam as-Sheikh Muhammad ibn Swaaleh al-Uthaymeen (rahimahullaah) akiulizwa maswali –na walikuwa pamoja naye shaykh Allamah Rab'i ibn Haadi na Shaykh Ali al-Halabi- akajibu [Shaykh Uthaymin] baadhi ya maswali, na akasema [kujibu mengine] :

'Muulizeni Yule bahri (bahari ya ilmu)!' Na kuashiria kwa sheikh wetu Ali al-Halabi (hafidhahullaah)!!"

3. Imaam Muhammad Naasir-ud-Deen Al-Albani (rahimahullaah)

1. Alisema katika kitabu chake maarufu 'Silsilah as-Swahihah : 2/720', alipokuwa akibainisha uovu wa mpinzani wa sunnah na hadîth 'Hasan AbdulMannan' , Alisema [Shaykh Al-Albaani] : "…na urefu wa kubainisha aibu ya maneno yake [AbdulMannan] katika kuzidhoofisha hadithi hizi; inahitaji kitabu pekee, na haya ni katika mambo ambayo wakati wangu hauniruhusu, nataraji labda baadhi ya ndugu zetu waliomakinika katika ilmu hii wanawaeza kufanya hivyo: kama ndugu Ali Al-Halabi."

[1] Katika ziyara zake za mjini Toronto, Canada; nilimuuliza sheikh Ali kuhusu mwanachuoni huyu mkubwa [Hammad al-Answaaree ; ambaye asili yake ni nchi ya Mali, Afrika magharibi], hivyo akanieleza sheikh Ali kuwa alikutana naye sheikh Hammad, na akampa hiyo ijaazah.

2. Alipozungumza (uovu) Abu Ruhaym kuhusu Shaykh Ali Al-Halabi, katika maneno aliyosema Imaam Al-Albaani kumuambia abu ruhaym:

“Ikiwa aqida yako ni kama aqida ya masheikhe watutu ambao [unadai] unawatetea, nao ni Ibn Baaz, Ibn Uthaymin, na Albaani, basi aqidah ya ndugu Ali [Al-Halabi] ni sawa na aqidah ya hao masheikhe watatu!!

Na ikiwa aqidah yako si kama aqidah ya ndugu Ali, basi mimi niko tayari kukaa na wewe!!!”

Maneno haya yalisemwa na ustadh Abu Abdullaah al-azami al-Jawaabira katika jawabu yake tarehe 20/Rabiul Awwal/1422, na ilishuhudiwa na ndugu Laafi as-Shatraat na Kaamil al-Qasshash.

3. Na akasema pia al-akh [ndugu] al-azami al-Jawaabira katika kitabu chake *‘Ni nini wanachokipinga kwa Imaam Al-Albaani, ukurasa 14:’*

‘Na nilimuuliza ustadh wetu shaykh Naasir [Albaani] : ‘Rai yako ni nini katika khilafu aliyokuja nayo Abu Ruhaym dhidi ya shaykh Ali Al-Halabi?’

Akajibu sheikhe wetu –kwa tamko moja- na Allaah ni shahidi wa ninayosema : ‘Al-akh [ndugu yetu] Ali ni kama abu ruhaym elfu moja!!!’

4. Na ni fakhri kubwa ya kuwa sheikhe wetu Ali Al-halabi ndiye sheikhe na mtu pekee aliyeandika utangulizi wa kitabu chochote cha Imaam Al-Albaani! Na kwa idhni ya Imaam Al-Albaani!!

5. Na kwa hakika sifa za Imaam Al-Albaani kwa sheikh wetu ni nyingi –walhamdulillaah-. Ukisikiza kanda za Imaam Al-Albaani utasikia mara nyingi akisema: ‘Yuko wapi Abul Harith?’ ‘Wacha tumsikiza Abul Harith,’ ‘Ama sivyo ewe Abul Harith,’ ‘Abul Harith alikuwa ataka kuongeza’ ……!!!

4. Shaykh Al-Allaamah Muqbil al-Waadi’ (rahimahullaah)

Aliulizwa shaykh Muqbil kama katika kitabu *chake ‘Tuhfatul Mujib, ukurasa 160’* :

Ni ma Ulamaa gani unaotunasihi tuwategemee na kusoma vitabu vyao na kusikiza kanda zao?

Akajibu (rahimahullaah):

‘Tushazungumza kuhusu jambo hili mara nyingi, lakini tutaregelea tena: katika wao ni Sheikh Naasir-ud-deen Al-Albaani, na wanafunzi wake wafadhili kama ndugu **Ali ibn Hasan ibn Abdulhamid….’**

Na pia alisema shaykh Muqbil [mahala pengine] : 'Na nimeona kitabu kizuri kinachoitwa: *'Fiqhul waaqi' bayna an-Nadhwariyya wa Tatwbiq'* -cha ndugu yetu kwa sababu ya Allaah- Ali ibn Hasan ibn Abdulhamid, Tunawanasihi mukisome na mukitegemee, na Allaah amjaze kheri.'

Na pia alitaja kitabu hichi katika kitabu chake [shaykh Muqbil] *'Ghaaratul Ashrita…'* na akasema kuhusu kitabu hicho [cha sheikh Ali]: 'Sijaona kitabu chochote kama hicho!!!'

6. Shaykh al-Muhaddith Abdulmuhsin Al-Abbaad (hafidhahullaah)

1. Alisema sheikh Amjad salhub: 'Tulikuwa katika Umra mimi na baadhi ya ndugu zetu, hivyo tukamtembelea sheikh Abdulmuhsin Al-Abbaad (hafidhahullaah), na katika maswali yaliyoulizwa, nilimuuliza sheikh: 'Sisi twatoka ardhi ya Shaam, ni nani unayetunasihi katika ma Ulamaa wake?'

Akajibu: **'Shikamaneni na sheikh Ali Hasan.'**

2. Na katika kitabu chake chenye manufaa mengi *'Rifqaan Ahlus-Sunnah',* chapa ya pili ukurasa 8-9, alisema:

'Na nawapa wasiyya tullabul ilm [wanafunzi] wote katika kila mji wajinufaisha na wale [masheikhe] wanaojishugulisha na ilmu [katika] Ahlus-Sunna katika miji yao, kama wanafunzi wa sheikh Albaani (rahimahullaah) huko Jordan, ambao walifunguwa markaz kwa jina lake [Imaam Albaani]….'

Juhudi Zake Katika Da'wah:

- Ni katika waanzishi wa 'Markaz al-Imaam Al-Albaani' , markaz ya ki ilimu huko Ammaan, Jordan

- Ni katika waanzishi wa jarida la 'Al-Aswaalah', lilikuwa likichapishwa Ammaan [na kusambaa miji ya mbali], naye alikuwa ni katika waandishi na wahariri vile vile.

- Alikuwa akiandika makala katika jarida la 'Al-Muslimun', lilikuwa likichapishwa London, kila wiki. Hii ilianza mnamo Rabiul Awwal 1417 Hijri na ikaandelea kwa muda wa miaka miwili.

- Anashiriki katika mihadhara mengi ya kiislaamu katika miji tofauti : Amerika, Canada, Uingereza, Holland, Indonesia, France na kwengineko.

Vitabu Vyake:

Kwa uhakika sheikh Ali Al-Halabi juhudi zake zinamsifu; bila ya kuongeza maneno. Ameandika na kuhakikisha zaidi ya vitabu mia mbili (200)!!! Kati yao ni risala ndogo, na vyengine ni mijalada sita!! Baadhi ya vitabu hivo ni:

1. 'Ilm Usool Al-Bid'ah [Ilmu ya misingi ya bid'ah]

2. Diraasaat 'Ilmiyyah fee Saheeh Muslim

3. Ru'yatun Waaqi'iyyah fil-Manaahij ad-Da'awiyyah [Mwangalio wa kileo katika manhaj zinazotumiwa katika Da'wah]

4. An-Nukat 'alaa Nuzhat-in-Nadhar [

5. Ahkaam ash-Shitaa fee as-Sunnah al-Mutahharah

6. Ahkaam al-'Eidayn fee as-Sunnah al-Mutahharah

7. At-Ta'aleeqaat al-Athariyyah 'alal-Mandhoomah al-Bayqooniyyah

8. Ad-Da'wah ilaa Allaah baina at-Tajammu' al-Hizbee wat-Ta'aawun ash-Shar'ee

9. "Miftaah Daar as-Sa'aadah" ;ya Imaam Ibn Al-Qayyim [mijalada 3]

10. "At-Ta'aleeqaat ar-Raddiyyah 'alaa ar-Rawdat an-Nadiyyah" ya Al-Albaanee [mijalada 3]

11. "Al-Baa'ithul-Hatheeth" ; ya Ahmad Shaakir [mijalada 2]

12. "Al-Hittah fee Dhikri as-Sihaah as-Sittah" ; ya Sideeq Hasan Khaan [mjalada]

13. "Ad-Daa wad-Dawaa" ; ya Ibn Al-Qayyim [mjalada]

14. "Al-Mutawaaree 'alaa Abwaab Al-Bukhaaree" ; ya Ibn Al-Muneer [mjalada]

15. Ighaathatul-Luhfaan; ya Ibn Al-Qayyim [mijalada 3]

16. Taarikh Ahlul Hadith ; ya Ad-Dihlawi

17. Tahdhir min fitnatul Takfir ; ya Albani, Bin Baaz, na Uthaymin

18. At-Tuhaf min madhhab as-Salaf ; ya Shawkaani

19. Tadhkira fi Ulumul hadîth ; ya Ibn Mulaqqin

20. Ta'leeq ar-Radhwiyya ala Rawdhatun-Nadiyya ; ya Siddiq Hasan Khan, Albaani [mijalada 3]

21. Riyaadhu-s-Swalihin ; ya An-Nawawi

22. Sunan Ibn Maajah [mijalada 3]

23. Al-Ubudiyyah ; ya Ibn Taymiyyah

Huu ni wasifu mfupi wa sheikhe wetu ; Ali Hasan al-Halabi al-Athari.

Tunamuomba Allaah ampe –yeye na sisi- mema ya dunia na akhera, na amlekeza katika kila la kheri na usawa.

Amin.

Imetayarishwa na Abdulazeez,

Toronto, Canada.

24 Jumadaa at-Thaani 1430.